
# KUCHELEWA KUOA NA KUOLEWA

**Je Faida na Hasara zake ni Zipi?**




Mwandishi: Simon Lucian Mathew

Anuani: Po Box 12, Ziba- Tabora

Mawasiliano: 0787 011 055

Email: simonlucian816@gmail.com

## SHUKRANI

Kwanza kabisa napenda Kumshukuru Mungu kwa kunipa uhai na uzima wa mwili pamoja na akili, pia kuniwezesha kukamilisha kazi hii ya Uandishi.

Pili, Ningependa kuishukuru Familia yangu kwa ushirikiano wa dhati na kuniunga mkono wakati wa mchakato wa kuandika kitabu hiki. Baba yangu Bw. Lucian Mathew na Mama yangu Mrs Lucian mumekuwa na mchango mkubwa sana hasa katika kunifundisha na kunielewesha mambo mengi kuhusu maisha ya ujana hadi Ndoa kwa ujumla. Elimu yenu ndio imeniwezesha hasa kuandika kitabu hiki.

Pia, nawashukuru Marafiki zangu wa karibu (Tatu khatibu,Bw. Max, Erasto Mapinduzi, na wengine wengi) kwa moyo wao wa kusaidia na kutoa mawazo muhimu yaliyowezesha kufanikisha kazi hii.

Ningependa kutoa shukrani za pekee kwa Mwalimu wangu/Rafiki yangu ambaye amekuwa Msukumo mkubwa kwangu Katika kufanikisha jambo hili, kwa kutoa mchango wa mawazo toka mwanzo hadi mwisho wa kazi hii. Mungu akubariki sana rafiki yangu.

Asante pia kwa wasomaji wangu wote kwa kunihamasisha na kunipa nafasi ya kushiriki somo Hili na ulimwengu.

Ninafurahi sana kwa mchango wa kila mtu katika kufanikisha kitabu hiki " ASANTENI SANA"

# YALIYOMO

**SHUKRANI……………………………………………………………………………………………………………………………………I**

NINI MAANA YA KUOA NA KUOLEWA? ······ 1

KWA NINI SIKU HIZI VIJANA WAMEKUWA HAWATAKI KUOA NA KUOLEWA? NA IKITOKEA AMEOA AU AMEOLEWA NI KWA KUCHELEWA SANA ······ 3

Je, kuna faida zozote zinapatikana kutokana na tabia ya kuchelewa kuoa au kuolewa? ······ 3

Hapa chini ni baadhi ya faida na hasara za kuchelewa kuoa. ······ 3

Faida ······ 3

Vipi kuhusu hasara, je KUCHELEWA KUINGIA KWENYE NDOA KUNA HASARA? ······ 3

Hasara/Athari ······ 3

Vitu vya kuzingatia kabla ya kuoa……………………………………………………………………………4

Vitu vya kuzingatia kabla ya kuolewa………………………………………………………………………5

Kijana unayechelewa kuoa piga hesabu zifuatazo…………………………………………………………6

Naomba upige kidogo hizi hesabu……………………………………………………………………………7,8,9

MR. SIMON LUCIAN MATHEW

# Nini Maana ya Kuoa au Kuolewa?

## UTANGULIZI

Kuoa ni kitendo cha mume na mke kuungana kisheria na kuishi pamoja kama familia moja. Kuolewa ni kitendo cha mwanamke kuolewa na mume na kuishi pamoja kama familia moja.

*Kwa nini vijana huoa?*

- Vijana huoa kwa sababu wanataka kuendeleza vizazi vyao na kutafuta mwenzi wa kuishi naye maisha yao yote.

*Kwa nini mabinti huolewa?*

- Mabinti huchagua kuolewa kwa sababu wanataka kuanzisha familia na kuishi na mume maisha yao yote.

- Kuoa au kuolewa ni utekelezaji wa wito wa asili KIMUNGU na kitamaduni pia, wa kutafuta mwenzi wa kuishi naye maisha yako yote.
- Kuendeleza familia ni moja ya sababu kuu ya vijana kuoa na mabinti kuolewa.
- Pia, wengi wanatafuta usalama wa kihisia na kifedha katika ndoa.
- Kwa wengine, ni sehemu ya tamaduni au dini zao.

- Hata hivyo, ni muhimu kukumbuka kwamba kuoa au kuolewa sio lazima kwa kila mtu na inapaswa kuwa na uamuzi wa hiari wa watu binafsi.
- Ni muhimu pia kuheshimu maamuzi ya wale ambao hawajachagua njia hiyo ya maisha.

## Vitu Vya Kuzingatia Kabla Ya Kuolewa

Kabla ya kuolewa, kuna vitu kadhaa ambavyo ni muhimu kuzingatia ili kuhakikisha ndoa yako inakuwa ya mafanikio. Hapa chini ni baadhi ya vitu unavyoweza kuzingatia:

- ✧ Kujiandaa kiakili na kiuchumi: Ndoa inahitaji maandalizi ya kiakili na kiuchumi. Hakikisha unaelewa majukumu yako kama mume au mke na una uwezo wa kifedha wa kutoa mchango wako katika ndoa.
- ✧ Kuelewa na kuheshimu tamaduni na mila za mwenzi wako: Kabla ya kuolewa hakikisha unaelewa na unaheshimu tamaduni na mila za mwenzi wako. Hii itasaidia kuzuia migogoro ya kiutamaduni katika ndoa yenu.
- ✧ Kujenga urafiki mzuri na mwenzi wako: Urafiki mzuri ndiyo msingi wa ndoa ya mafanikio. Hakikisha unatumia muda wa kutosha kujenga urafiki mzuri na mwenzi wako kabla ya kuingia katika ndoa.
- ✧ Kuzungumza kwa uwazi na mwenzi wako: Kabla ya kuolewa hakikisha unajifunza kuzungumza kwa uwazi na mwenzi wako. Mawasiliano mazuri ni muhimu sana katika ndoa ya mafanikio.
- ✧ Kujifunza kusamehe na kusahau: Hakuna ndoa ambayo haina migogoro. Ni muhimu kujifunza kusamehe na kusahau makosa ya mwenzi wako ili kuzuia migogoro kuwa kikwazo katika ndoa yenu.

KUMBUKA; Kuzingatia vitu hivi kabla ya kuolewa kutakusaidia kuanza ndoa yako kwa mafanikio na furaha.

MR. SIMON LUCIAN MATHEW

KWA NINI SIKU HIZI VIJANA WAMEKUWA HAWATAKI KUOA NA KUOLEWA? NA IKITOKEA AMEOA AU AMEOLEWA NI KWA KUCHELEWA SANA

# JE, KUNA FAIDA ZOZOTE ZINAPATIKANA KUTOKANA NA TABIA YA KUCHELEWA KUOA AU KUOLEWA?

- HAPA CHINI NI BAADHI YA FAIDA NA HASARA ZA KUCHELEWA KUOA.

FAIDA

- Kupata muda wa kujitambua: Vijana na mabinti ambao hawajaolewa wanapata nafasi ya kujifunza zaidi kuhusu nini wanataka katika maisha yao na kujenga utambulisho wao binafsi.
- Kufurahia uhuru: Kwa kuwa hawajaolewa, vijana na mabinti wana uwezo wa kufanya mambo wanayopenda bila kujali maoni ya wengine au kutegemea idhini ya mwenzi(mke/mume)
- Kujenga uhodari wa kifedha: Kuchelewa kuoa kunaweza kutoa nafasi ya kuwekeza katika kazi au biashara yako na kuwa tajiri, ambayo inaweza kufaidisha katika ndoa yako baadaye.

VIPI KUHUSU HASARA, JE KUCHELEWA KUINGIA KWENYE NDOA KUNA HASARA?

Kuchelewa kuoa kuna athari mbalimbali kwa vijana na mabinti,Zifuatazo ni baadhi

HASARA/ATHARI

- Uchovu: Vijana na mabinti wanaweza kuchoka kusubiri mwenza wake kwa muda mrefu na kujisikia peke yao. Inaweza kusababisha kuwa na wasiwasi wa kuolewa na hata msongo wa mawazo.

MR. SIMON LUCIAN MATHEW

- Kupoteza nafasi ya kupata mwenzi mzuri: Kuchelewa kuoa kunaweza kusababisha vijana na mabinti kupoteza nafasi ya kuolewa na mwenzi ambaye wanapenda na wanafaa nao.
- Upungufu wa uzazi: Vijana na mabinti wanapopata mtoto katika umri wa makamu na baadaye, inaweza kuwa ngumu kupata watoto na hata kuongeza hatari ya matatizo ya uzazi.

KUMBUKA; Umri wa Makamo ni miaka (35-45).Kwa hiyo, ni muhimu kwa vijana na mabinti kuzingatia faida na hasara hizi kabla ya kufanya uamuzi wa kuoa au kuchelewa kuoa.

## Vitu Vya Kuzingatia Kabla Ya Kuoa

Kabla ya kuoa ni muhimu kuzingatia mambo yafuatayo:

1. Kumjua vizuri mwenzi wako - Ni muhimu kumfahamu mwenzi wako kwa undani kabla ya kuoa ili kuepuka masuala ya kushangaza baadaye.

2. Uwezo wa kifedha - Ni muhimu kuhakikisha una uwezo wa kifedha wa kutosha kwa ajili ya kuanza familia.

3. Maoni ya familia - Ni muhimu kuhakikisha familia zenu zinaelewana na mnakubaliana na uamuzi wa kuoa.

4. Ubunifu wa maisha - Kabla ya kuoa ni muhimu kuwa na mpango wa maisha wa pamoja ili muweze kuzingatia mipango ya kifedha.

5. Mipango ya baadaye - Ni muhimu kuwa na mipango ya baadaye kwa ajili ya mustakabali wa familia kama vile kupanga familia, elimu, na maendeleo ya kazi.

Kwa kuzingatia mambo haya, utakuwa na maandalizi mazuri kwa ajili ya ndoa yako.

MR. SIMON LUCIAN MATHEW

## Vitu Vya Kuzingatia Kabla Ya Kuolewa

Kabla ya kuolewa, kuna vitu kadhaa ambavyo ni muhimu kuzingatia ili kuhakikisha ndoa yako inakuwa ya mafanikio. Hapa ni baadhi ya vitu unavyoweza kuzingatia:

- Kujiandaa kiakili na kiuchumi: Ndoa inahitaji maandalizi ya kiakili na kiuchumi. Hakikisha unaelewa majukumu yako kama mume au mke na una uwezo wa kifedha wa kutoa mchango wako katika ndoa.
- Kuelewa na kuheshimu tamaduni na mila za mwenzi wako: Kabla ya kuolewa hakikisha unaelewa na unaheshimu tamaduni na mila za mwenzi wako. Hii itasaidia kuzuia migogoro ya kiutamaduni katika ndoa yenu.
- Kujenga urafiki mzuri na mwenzi wako: Urafiki mzuri ndiyo msingi wa ndoa ya mafanikio. Hakikisha unatumia muda wa kutosha kujenga urafiki mzuri na mwenzi wako kabla ya kuingia katika ndoa.
- Kuzungumza kwa uwazi na mwenzi wako: Kabla ya kuolewa hakikisha unajifunza kuzungumza kwa uwazi na mwenzi wako. Mawasiliano mazuri ni muhimu sana katika ndoa ya mafanikio.
- Kujifunza kusamehe na kusahau: Hakuna ndoa ambayo haina migogoro. Ni muhimu kujifunza kusamehe na kusahau makosa ya mwenzi wako ili kuzuia migogoro kuwa kikwazo katika ndoa yenu.

MR. SIMON LUCIAN MATHEW

MR. SIMON LUCIAN MATHEW

## KIJANA UNAYECHELEWA KUOA PIGA HESABU ZIFUATAZO

Kuna namna flani hivi kumekua na uzito mkubwa kwa vijana wetu kuoa na baadhi yao wamekua wakioa muda umeshaenda sana!

Kuna siku nilikua natafakuri juu ya hili na nikawaza sana juu ya jambo hili ndipo leo nimesukumwa angalau nitoe mawazo yangu juu ya jambo hili ambalo linakua kwa kasi Huenda vijana wetu hawajui athari za kuoa muda umeenda na huenda wanachukulia kawaida sana juu ya jambo hili

- Huenda hawalipi kipaumbele sana kama mambo mengine na nikama suala la kuoa linapoteza mvuto kwa vijana wetu.
- Nakumbuka zamani kidogo vijana tulikua tunawiwa sana kuoa na tulikua na shauku kubwa sana ya kupata mwenza ili maisha yazidi kusonga mbele zaidi.
- Kijana alikua akioa tunamtamania kwelikweli na kuzidisha hamasa ya kupata mke, lakini kwa sasa nikama vile hayo mambo yanapotea sana.

Hata kama kijana anaoa vijana wenzake wanachukulia kawaida sana na ni kama vile wanamwonea huruma kwanini amejiingiza huko.

Bado wanaume ambao wako kwenye ndoa utawasikia wakiwakaribisha vijana ambao wameoa kwa masikitiko makubwa, "eti ooh karibu kwenye chama chetu" wanavyoitamka ni kama vile kinafiki hivi.

- Siku hizi kijana akinunua iphone au smart kali sana utasikia akishangiliwa sana na kuonewa wivu lakini si upande wa kupata mke, hapa atazomewa na kuona kama vile amepotea.

Cha ajabu ni kwamba na yeye kuna siku ataoa tu hasa baada ya umri kwenda.

## NAOMBA UPIGE HIZI HESABU KIDOGO

(a) Hoja ya kwanza: Namna ambavyo utawasomesha watoto wako

- kwa mfano umeoa ukiwa na umri wa miaka 35, kwa neema ya Mungu tunatarijia utapata mtoto ukiwa na miaka 36. Ataanza chekechea ukiwa na umri wa miaka 40 na atamaliza darasa la saba ukiwa na umri wa miaka 47. Atamaliza kidato cha nne ukiwa na umri wa miaka 51 na atamaliza kidato cha sita ukiwa na umri wa miaka 53, kama wewe ni mtumishi wa serikali umeshaanza kuwaza kustafu. Na atamaliza chuo kikuu (shahada ya kwanza) ukiwa na umri wa miaka 56 au 57. Kumbuka hizi hatua zote mtoto bado anakutegemea wewe umtunze na kumsomesha.
- Hapa ulishaanza kuitwa babu na ni mzee sasa, kumbuka huyo ni mtoto wako wa kwanza, kama watapishana kwa miaka mitatu mitatu watoto wako, kwahiyo mtoto wako wa pili ili amalize chuo basi wewe utakua na miaka 60, watatu miaka 63 na wanne miaka 66.
- Kwahoja kama hizo utajikuta uzee wako wewe badala ya kula uzee basi utakua unahangaika kusomesha na kutunza watoto wako.

MR.SIMON LUCIAN MATHEW

- Hutafaidi matunda ya watoto wako maana mpaka wajipange na wawe na maisha yao basi ulishakua mzee kwelikweli!

(b) Hoja ya pili: Namna ambavyo utampata mke wako.

- Kwanza kabisa fikiri hili, kwa wasichana wanakuwa tayari kuolewa wakiwa kati ya miaka 22-30 na asilimia kubwa sana huolewa kwenye umri huo.Hoja yangu hapa ni kwamba itakua ngumu sana kupata mke ambaye mtaendana kiumri, ni ngumu sana kama una mika 35 kumpata binti wa miaka 33 au 32 ili kuleta uwiano wa kiumri. itakua ngumu sana kupata binti labda "wanawake" na hii ni kutokana na aina ya kizazi tulichonacho.
- Kwahiyo utalazimika kuoa binti wa miaka 25 ambaye utakua unamzidi miaka 10, na hapa mara nyingi sana unakuta mpishano ni wa hali ya juu sana maana wakati wewe unawaza maisha yeye anawaza "ale ujana kwanza", unamwambia tufanye hiki na kile yeye anasema mume wangu tutafanya tu. Ebu kumbuka hili, wakati ulipokua na miaka 25 je ulikua unaweka uzito mkubwa sana kwenye maisha yako ya baadae? je ulikua unaweka uzito mkubwa kama wa sasa hivi? kwahiyo kumbuka huyo binti mambo mengi atakua haweki uzito sana (japo siyo wote lakini wengi wako hivyo)Itakua ngumu sana kumtosheleza kwenye tendo la ndoa maana wewe tayari umri wako umesogea sana na yeye bado damu inachemka sana, anataka "dozi kubwa kubwa" na wakati wewe una mambo mengi na dozi yako imeshaanza kupungua.

Hizo ni hoja chache ambazo zinaweza kukusogeza kwenye kufanya maamzi juu ya umri wako wa kuoa, asante sana na Mungu akubariki sana.

MR. SIMON LUCIAN MATHEW

VYANZO

- Maarifa kutoka kwa Wazee wetu
- Maarifa kutoka Social Media (Twitter, Facebook nk)
- Mawazo kutoka kwa rafiki zangu

MR. SIMON LUCIAN MATHEW